



Maandishi ya CIE ya Idhini ya Simu (Kiswahili)

Anza Maandishi ya Ridhaa

Una haki ya kutoa ridhaa kwenye karatasi. Je, unakubali kutoa ridhaa yako katika muundo huu uliorekodiwa wa kielektroniki?

Ikiwa “ndiyo” endelea

Ikiwa “la” usiendeleo

Taarifa hii inaiidhinisha Community Information Exchange kuunda rekodi na kushiriki taarifa binafsi, fedha, na za afya zilizoshirikiwa nasi na Washirika wetu wa Rufaa. Kwa kutoa ridhaa yako, unaiidhinisha mahususi CIE kutumia na kufichua taarifa kuhusiana na Matumizi Mabaya ya Dawa za Kulevya/Pombe/Vileo, Afya ya Akili, VVU/UKIMWI.

Taarifa hii itatumika kutathmini mahitaji yako na kuratibu utunzaji wako. Katika baadhi ya hali, taarifa yako inaweza kufichuliwa upya na isiwe tena inalindwa chini ya sheria za faragha zinazotumika.

Hata hivyo, taarifa yako bado itakuwa imelindwa chini ya Makubaliano yetu ya Ushiriki pamoja na washirika wetu. Kukataa kwako kutupatia ruhusa ya kushiriki taarifa yako hakutaathiri matibabu yako, malipo, usajili au ustahiki wa kupokea mafao kutoka kwa Washirika wetu wa Rufaa. Tafadhali nenda kwenye tovuti yetu: www.ciesandiego.org/privacy, ili kupata orodha ya Washirika wetu wa Rufaa, na Ilani yetu ya Mazoea ya Faragha ili kujifunza jinsi tunavyotumia na kushiriki taarifa yako, na jinsi ya kupata nakala au kufutilia mbali idhini hii, ambapo una haki ya kufanya hivyo wakati wowote. Ukifutilia mbali idhini hii, haitaathiri taarifa ambayo tayari imeshirikiwa.

Idhini yako itakuwa halali kwa muda wa miaka kumi kuanzia tarehe ya leo, isipokuwa ukiifutilia mbali mapema.

Kama sahihi yako ya kielektroniki na makubaliano, tafadhali andika: jina lako, tarehe ya kuzaliwa na tarehe ya leo.

Mwisho wa Maandishi

Nimemsomea mteja Idhini ya CIE na amekubali kushiriki taarifa zake za mahitaji yake ya kijamii na kiafya, akijua kwamba sikuweza kupata sahihi yake. Kama mbadala wa sahihi, ninapakia hati hii kama uthibitisho.